



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**  
**BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA**



**07 Januari, 2026**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**  
**KUSOGEZWA MBELE KWA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA UMOJA**  
**WA GOFU WANAWAKE TANZANIA (TLGU)**

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linapenda kuwataarifu wanachama na wadau wa Umoja wa Gofu Wanawake Tanzania (TLGU), kuwa uchaguzi wa viongozi wa umoja huo uliotarajiwa kufanyika tarehe 10 Januari, 2026, utafanyika tarehe 7 Februari, 2026 Jijini Dar es salaam.

Vile vile muda wa kuchukua na kurudisha fomu umeongezwa hadi tarehe 5 Februari, 2026, Fomu zinaendelea kutolewa katika Ofisi za BMT zilizopo Uwanja wa Benjamin Mkapa na zinapatikana katika tovuti ya Baraza ambayo ni [www.bmt.go.tz](http://www.bmt.go.tz).

Aidha, Usaili wa wagombea wa nafasi tofauti utafanyika tarehe 06 Februari, 2026 katika Ofisi za Baraza la Michezo la Taifa.

Nafasi zinazogombewa katika uchaguzi huo ni pamoja na:

**Nafasi**

1. Rais
2. Makamu wa Rais
3. Katibu wa Heshima
4. Mhazini wa Heshima
5. Katibu wa Mashindano
6. Katibu wa Handicap

**Ada**

50,000/=

**Sifa za wagombea**

- i. Awe Raia wa Tanzania
- ii. Awe na elimu isiyopungua Kidato cha nne (cheti cha Elimu ya Sekondari)
- iii. Awe na ujuzi na uzoefu wa uendeshaji wa michezo wa golf uliothibitishwa wa angalau miaka miwili (2).
- iv. Awe anazifahamu sheria za mchezo wa gofu
- v. Awe na umri usiopungua miaka ishirini na tano (25)
- vi. Awe amewahi kuwa ama mchezaji wa golf, Kocha, Mwamuzi, Kiongozi au kushiriki katika uendeshaji wa mchezo wa golf.
- vii. Awe na uwezo wa kutatua changamoto.

Malipo ya fomu yafanyike katika akaunti ya Baraza, kwa kutumia mfumo mpya wa malipo ya Serikalini.

Ili kupata namba malipo mgombea anashauriwa kupiga namba ya simu ifuatayo; 0683 578 186

Aidha, fomu ya kugombea iwasilishwe Baraza ikiambatishwa na risiti ya malipo pamoja na nakala za nyaraka kulingana na sifa mahususi zilizoainishwa katika katiba ya TLGU.

BMT inatoa wito kwa yeyote mwenye sifa kwa mujibu wa katiba ya chama cha mchezo wa golf Wanawake kujitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya uchaguzi huo na maendeleo ya Mchezo huo nchini.

**Imetolewa na:**

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**